ISO 9001:2015 Certificate

Linatolewa bure

# The Regulator

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISSN: 0856 - 8030 NA. 4/2023 OKTOBA - DESEMBA 2023




KUMBUKIZI MIAKA 20
TCRA

**Mafanikio na mwelekeo wa usimamizi**

# TCRA mwezeshaji Uchumi wa Kidijitali



# Matumizi Salama ya Mtandao kwa Wazee

## Dondoo

**ZINGATIA**
Kuwa makini na maudhui unayoweka kwenye mtandao.

**HUISHA:**
Mifumo ya kifaa chako cha mawasiliano mara kwa mara.

**NYWILA:**
Tumia nywila imara ambayo unaweza kukumbuka kwa urahisi.

**BOFYA:**
Chukua tahadhari. Usifungue viunganisho (link) ambavyo hutambui chanzo chake.

**LINDA:**
Taarifa zako za mawasiliano na chukua tahadhari za ziada.

tcra_tanzania

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 4/2023. OKTOBA - DESEMBA, 2023

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## TCRA ina wajibu katika majukumu yafuatayo:-

1. Kuhimiza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda haki na maslahi ya watumiaji;
3. Kuhamasisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wote (wakiwemo Walemavu) ukijumuisha watumiaji wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji ambao wako katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara;
4. Kuimarisha elimu kwa umma, uelewa na kuzifahamu huduma zinazosimamiwa;
5. Kuhakikisha umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Dkt. Peter Kihogo
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz;
dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

**Ofisi Kuu**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu +255 784 558270-1 Simu ya bure: 0800008272.
Barua pepe: dg@tcra.go.tz. Tovuti: www.tcra.go.tz

**Ofisi ya Zanzibar**
Na. 19 Mbuyukisutu, Mjini Magharibi, Zanzibar.
S.L.P 3284,
Postikodi 71194 Mjini Magharibi
Simu: +255 24 2235062
Baruapepe: zanzibar@tcra.go.tz

**Kanda ya Kaskazini**
Jengo la PAPU, Ghorofa ya kumi na mbili. 280 Barabara ya Moshi-Arusha. S.L.P 15675,
Postikodi 23194 Arusha.
Simu: +255 272970286
Baruapepe: arusha@tcra.go.tz

**Kanda ya Kati**
LAPF Plaza, Ghorofa ya nne. Na. 2 Mtaa wa LAPF.
S.L.P 2229,
Postikodi 41194 Dodoma. Simu: +255 262321731
Baruapepe: dodoma@tcra.go.tz

**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya tano. Na. 7 Barabara ya Karume.
S.L.P 1375,
Postikodi 53194 Mbeya. Simu: +255 25 250 5016
Baruapepe: mbeya@tcra.go.tz

**Kanda ya Ziwa**
Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya nne, upande B Na.13
Jomo Kenyatta Avenue.
S.L.P 3108,
Postikodi 32194 Mwanza. Simu: +255 28 2505082,
Baruapepe: mwanza@tcra.go.tz

**Kanda ya Mashariki**
Na.147 Barabara ya Kajenge, Mikocheni,
S.L.P 35615,
Postikodi 14194 Dar es salaam.
Simu: +255 22 2775110
Baruapepe: easternzone@tcra.go.tz

# Yaliyomo


04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu






13 Mfumo wa leseni ulivyochochea huduma za mawasiliano






06 TCRA kama mwezeshaji Uchumi wa Kidijitali

Makala kuu


16 Takwimu sekta ya Mawasiliano



09 Tunu za usimamizi na ustawi wa Watanzania





22 Majiji ya kidijitali ajenda mkutano wa ITU Arusha




# Jielimishe kwa kupata nakala za Regulator bure

Jarida hili ni mojawapo ya nyenzo zinazotumiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuongezaa kiwango cha elimu ya umma na uelewa wa masuala ya sekta zinazosimamiwa, zikiwemo mawasiliano ya simu, huduma za posta na utangazaji.

Jarida hili la kila robo mwaka pia linawezesha kueneza taarifa muhimu kuhusu majukumu ya TCRA. Regulator sio tu chapisho: ni jukwaa linalowezesha uwasilishaji wa maudhui yanayoingia kwa undani kwenye ulimwengu wa mawasiliano.

Regulator lina maudhui yaliyotafitiwa vizuri na kwa undani kwa madhumuni ya kuwawezesha wasomaji kupata habari za masuala yanayojitokeza kwenye sekta ya mawasiliano ya kielektroniki na posta.

Linafafanua masuala haya,yakiwemo tekinolojia mpya na mabadiliko kwenye sera na mifumo ya usimamizi pamoja na namna hali ya soko la mawasiliano inavyobadili sekta.

Jarida limesanifiwa upya, kuwezesha wasomaji kupata maudhui kwa urahisi na lina michoro, picha, makala fupi na uchambuzi. Lina mwelekeo mpya, uchambuzi wa ndani na maudhui yanayofikirisha na kutia moyo.

Maudhui ya jarida yanakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya. Jarida linawezesha na kuendeleza mijadala kwenye sekta ya mawasiliano. Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu.

Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tafadhali tuma barua pepe kwa: barua@tcra.go.tz. Kwa maelezo zaidi, piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni 0800008272.






UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# Kuendeleza fursa za kidijitali kwa wote



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

*Ujumbe huu ulitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari siku ya Mawasiliano ya Simu Afrika, 7 Desemba 2023*

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina majukumu makubwa katika kujenga mazingira wezeshi ya kuendeleza mawasiliano ya simu na teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ujumla nchini.

TCRA inaweka na kusimamia mfumo wa usimamizi wa sekta ya mawasiliano kwa ufanisi kwa lengo la kuendeleza ushindani, uvumbuzi na upatikanaji wa fursa za kidijitali kwa wote. Wajibu huu unahusisha pia kuchochea ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ya simu maeneo ya pembezoni na kuhimiza mipango ya kujenga uelewa wa masuala ya kidijitali kwa wananchi na watumiaji.

TCRA inaweka mazingira wezeshi ya usimamizi, inahimiza mipango shirikishi na inashirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba matunda ya mapinduzi ya kidijitali yanasambazwa kwa wote, na hasa kuyafikisha kwa jamii ambazo hazipati huduma stahiki hapa Tanzania.

TCRA inatambua wajibu muhimu wa msimamizi katika kuchochea maendeleo ya sekta na kku0ndoa tofauti za upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano ya kisasa.

TCRA imeendelea kusimamia na kufuatilia miundombinu ya mawasiliano, ikijumuisha minara ya simu za mkononi, miundombinu ya waya za faiba na vituo vya kutunza data. Miundombinu hii ni muhimu kuelekea upatikanaji wa huduma za mawasiliano na matumizi yake sehemu mbalimbali nchini.

Serikali inatekeleza mipango ya kuendeleza TEHAMA na upatikanajiwa huduma kwa wote.

Hadi Septemba 2023 huduma za mawasiliano ya simu za mkononi zinazotumia teknolojia ya uzao wa tatu na wa nne, yaani 3G na 4G zilifika kwa asilimia 74 ya watu nchini. Kijiografia zilienea kwa asilimia 67 kwa 3G na asilimia 55 kwa 4G. Vifaa vya watumiaji pia vimeongezeka pia. Kwa mfano,simu za kawaida zinatumiwa na asilimia 83.6 ya watu na simu janja na asilimia 30.71.

Tunapofikia hatua hii ya maendeleo ya teknolojia, inatupasa kuhakikisha kwamba hakuna anayebaki nyuma.

Tanzania imejizatiti kuendeleza jamii shirikishi kidijitali, ambapo kila mtu ana fursa sawa wa kufaidi matunda ya TEHAMA.

Dhamira yetu sio tu kuunganisha watu lakini pia kuwawezesha kwa kuwaongezea uelewa wa masuala ya kidijitali, kuendeleza stadi zao na kuweka mazingira yanayochochea ubunifu na uvumbuzi.




*Washiriki wa uzinduzi wa Mwongozo wa Klabu za kidijiti*

Novemba 2023 TCRA ilizindua mwongozo wa vilabu vya kidijitali kwa lengo la kuwezwesha uanzishwaji na uratibu wa klabu hizo katoka shule, vyuo na vyuo vikuu nchini. Vilabu hivi vitachangia kupanua uelewa masuala ya TEHAMA na uchumi wa kidijitali, vitatoa fursaza kuendeleza stadi katika TEHAMA na zitawezesha kuimarika kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali Tanzania.

TCRA pia inawezesha watoa huduma kupanua huduma zao nchini.

Mnada wa masafa ya mawasiliano kwenye bendi za MHz 700, MHz 2300, MHz 2600, na MHz 3500 tarehe 11 Oktoba 2022 umewezesha watoa huduma kupanua wigo wa huduma za mawasiliano nchini.

Masafa hayo yanawezesha kuenea huduma zinazotumia teknolojia ya uzao wa tano, yaani 5G sehemu mbalimbali Tanzania.

Mkakati mwingine muhimu unaotekelezwa na TCRA ni mpango wa kutoa bila malipo na kwa vipindi maalum raslimali muhimu za mawasiliano kwa wavumbuzi wanaobuni huduma mpya za mawasiliano ili kufanya majaribio.

Raslimali hizi ni pamoja na namba, masafa na vikoa vya Tanzania.

**RIPOTI MAALUM:** Miaka 20 ya usimamizi bora

# TCRA kama mwezeshaji Uchumi wa Kidijitali

Na Mwandishi wetu

**Mwezi Novemba 2023, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inatimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake. Tunawaletea mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye eneo la usimamizi wa sekta kipindi hicho. Makala hii inaangalia historia ya Mamlaka hiyo na majukumu yake katika kufanikisha mipango ya maendeleo Tanzania.**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilianzishwa Novemba 2003 wakati wa kipindi muhimu kuliko vyote katika historia ya mawasiliano Tanzania. Kipindi hicho pia kilikuwa na umuhimu mkubwa kiteknolojia kwani kulikuwa na maendeleo na mabadiliko ya kasi.

Maendeleo ya teknolojia duniani yaliwezesha huduma za aina mbalimbali kuwa changamani. Kwa mfano, iliwezekana kutumia simu ya mkononi kwa huduma za ziada kama vile kutuma na kupokea data, kupata huduma za intaneti, kusikiliza redio na kufuatilia matangazo ya televisheni.

Hali hii ilitaka kuwe na muingiliano wa shughuli za usimamizi wa mawasiliano na utangazaji. Ilibidi wasimamizi wa sekta hizi ambazo awali zilijitegemea kuunganishwa. TCRA ilianzishwa katika muktadha huo.

TCRA ilitokana na kuunganishwa tume mbili za kimkakati, ambazo zilikuwa zinasimamia sekta zilizokuwa zinaunganika: Sekta ya Mawasiliano ya Simu, Intaneti na Posta na Sekta ya Utangazaji.

Tume ya Mawasiliano Tanzania (TCC) ilisimamia masuala ya simu, intaneti na posta, wakati Tume ya Utangazaji Tanzania (TCC) ikisimamia utangazaji, kwa Tanzania Bara. Zanzibar ina tume yake ya Utangazaji.

TCC na TBC zenyewe zilianzishwa kutokana na mabadilikop ya kiuchumi nchini, ambamo kampuni binafsi zilianza kushindana na zile za umma, kufuatia kulegezwa mashari ya uchumi miaka ya mwisho ya themanini na ya mwanzo wa tisini.

Kwa mfano, Shirika la Posta na Simu Tanzania, wakati ule likiitwa TPTC lilikuwa mtoa huduma pekee aliyetawala soko. Kwa utangazaji, Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ilikuwa na ukiritimba wa utangazaji, na miaka ya mwanzo ya tisini Tanzania Bara ilikuwa haina kituo cha televisheni. Zanzibar ilikuwa na televisheni iliyoanza 1974. Televisheni hii ya Zanzibar, ilikuwa televisheni ya kwanza ya Rangi, barani Afrika.

Mwezi Desemba 1993, TPTC iliyokuwa pia ni msimamizi, ilivunjwa na kukaundwa taasisi tatu, Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania (TPC) na TCC.



TBC ilianzishwa kusimamia masuala ya maudhui na utoaji wa leseni za huduma za redio na televisheni kwa upande wa Tanzania Bara.

Tume hizi zililenga kuendeleza dhana ya usimamizi huru wa sekta, yaani ambao unatenganisha udhibiti na masuala ya sera na utoaji huduma.

Usimamizi huru unaendeleza ushindani makini, unachochea ufanisi wa kiuchumi, unalinda maslahi ya

watumiaji wa huduma na bidhaa pia unawezesha ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji na utoaji huduma kwenye sekta.

TCC ilianza kutoa leseni za simu na huduma za data. Matumizi ya simu za mkononi yalienea mwaka 1994. Huduma hizi zilianza kwa mfumo wa analojia, teknolojia ambayo iliweka ukomo wa matumizi ya kifaa cha mawasiliano na baadae dijitali, unaowezesha huduma nyingi.

Mtandao unaojulikana sasa kwa jina la kibiashara la Tigo, ulikuwa wa kwanza. Ulifuatiliwa na Tritel, ambayo baadae ilisitisha huduma kwa sababu za kibiashara.

**1G**

Simu za mwanzo za mkononi, zikiwemo zilizoingia Tanzania mwanzoni, zilijulikana kama za uzao wa kwanza, au 1G. Hizi ziliwezesha maongezitu, ambapo simu haikuwa na uwezo wa kutuma ujumbe mfupi.

**2G**

Uzao wa pili, yaani 2G uliwezesha maongezi na kutuma meseji, au ujumbe na pia upeo mkubwa wa kuhifadhi data, ikiwa ni pamoja na majina.

Shughuli za utangazaji zilianza kupanuka kwa kuwa na redio na televisheni binafsi. TBC ilitoa leseni zilizowezesha kuanzishwa  televisheni za kwanza binafsi ambazo ni CTN Februari, 1994; ITV Mei, 1994; na DTV Desemba, 1994. Televisheni ya Taifa ilianza baadae. Jiwe la msingi la msingi la jengo la Televisheni ya Taifa liliwekwa tarehe 14 Aprili 1995.

Kwa ujumla, usimamizi unalenga kuendeleza sekta husika, kusimamia utoaji huduma na ushindani, kulinda watumiaji, kulinda watoa huduma; na kusimamia kanuni namiongozo.

Sekta ya mawasiliano inasimamiwa kwa kuwa ni muwezeshaji/mhimili wa sekta nyingine. Vilevile ni msingi katika maisha ya wananchi kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Sekta pia inahusu masuala ya teknolojia;  masuala ya tunu za taifa, zikiwemo utamaduni,mila,desturi. Ndiyo maana maudhui ya utangazaji yanasimamiwa na wasimamizi kote duniani.

Hata Marekani, Tume ya Mawasiliano ya taifa lile (FCC) ina majukumu ya kusimamia baadhi ya maeneo yanayohusu maudhui, hasa yanayoathiri watoto.

Mawasiliano pia yanasimamiwa kwa kuwa soko la huduma lina changamoto nyingi. Usimamizi vilevile unawezesha kudhibiti matumizi ya raslimali adhimu za taifa kama vile masafa na namba za mawasiliano.

Masafa yanatumika kusafirisha habari kwa njia mbali mbali kwa ajili ya kutoa huduma za simu, utangazaji na intaneti. Namba za mawasiliano zinapangwa kwa mantiki ili ziweze kutumiwa kwa urahisi, kutofautissha huduma na pia watumiaji.  Hizi ni pamoja na zile ndefu zinazotumika kwenye huduma za simu, namba fupi na misimbo ambayo inatumika kwenye miamala. Mfano ni misimbo inayoanza na *150*...#.

TCRA inasimamia sekta ya mawasiliano kwa kuandaa mipango ya kuendeleza sekta, kushauri serikali kuhusu masuala ya kisera, kuweka mifumo ya kanuni, kutoa leseni, kuongeza muda wake na hata kufuta inapobidi kwa mujibu wa kanuni.

TCRA pia inafuatilia ubora wa huduma kwa kutumia vigezo mbalimbali. Vigezo sita vya ubora wa huduma vinavyotumika na TCRA ni upatikanaji wa mtandao, unaopimwa kwa asilimia ya upatikanaji wa mtandao wakati watumiaji wanapohitaji huduma; kiwango cha simu zilizoshindwa kuunganishwa kuunganishwa kwenye mtandao; na kiwango cha simu zinazokatika kabla ya mazungumzo kukamilika na kabla ya wazungumzaji kukata simu kwa kukusudia.

Vigezo vingine ni jinsi watoa huduma walivyofikisha huduma husika, ubora wa sauti  na kasi kasi ya kusafirisha data katika mtandao.

TCRA pia inasimamia shughuli zitokanazo na matumizi ya vifaa vya mawasiliano, kama vile taka za elektroniki. Inaelimisha umma na watumiaji kuhusu masuala ya mawasiliano na teknolojia.Vilevile Mamlaka inatatua migogoro na malalamiko ya watumiaji. Inazo kamati mbalimbali kwa shuhuli hizi, zikiwemo Kamati ya Malalamiko na Kamati ya Maudhui.

TCRA imeainisha mikakati yake na ile ya kitaifa, kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya  maendeleo

2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III) kwenye sekta ya Mawasiliano.

Miaka 20 ya usimamizi wa sekta chini ya TCRA umewezesha Tanzania kujenga misingi ya kuingia uchumi wa kidijitali.

TCRA imefanikisha kuimarisha misingi mikuu ya uchumi huu ambayo ni miundombinu wezeshi; mifumo ya malipo, mifumo ya utambulisho wa watumiaji huduma kwa maana vitambulisho vinavyoweza kuhakikiwa, sera na mfumo wa iisheria na kanuni.

Mifumo ya malipo ni pamoja na kadi za malipo mtandaoni, benki na akaunti za pesa kwa simu za mkononi.

TCRA inahakikisha kwamba miundombinu ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA) Tanzania inaendeshwa na kusimamiwa vizuri.

Ukuzaji wa uchumi shirikishi na jumuishi unaowezesha upatikanaji wa huduma mtambuka za kiuchumi na kijamii kwa wananchi unahitaji mipango mizuri na usimamizi wa raslimali za mawasiliano kwa ufanisi.

# TCRA na uchumi wa kidijitali

Uchumi wa Kidijitali ni ule ambapo nchi inajenga mwelekeo tawala wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na mifumo ya kielektroniki kwenye sekta zote.

Uchumi wa buluu ni pale nchi zinapoweka mkazo kwenye matumizi ya rasilimali na fursa zinazotokana na Bahari au fukwe kujiendeleza kiuchumi.

Tanzania imejenga misingi yote na inakidhi mahitaji ya Uchumi wa kidijitali na wa buluu. Mahitaji hayo ni Pamoja na sera na mifumo wezeshi ya kisheria na kiusimamizi. Serikali imerekebisha sera za mawasiliano – zilizohusu sekta ndogo za TEHAMA, Posta na Utangazaji ili Kwenda na mwelekeo wa kiteknolojia duniani Uchumi wa kidijitali unategemea mifumo imara, salama na inayoaminika Pamoja na kupatikana huduma muhimu na kutumika kwake. Vilevile unahitaji uwepo wa mifumo salama ya malipo.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inachangia ujenzi wa Uchumi wa kidijitali na wa buluu kwa kuhakikisha kwamba shughuli zake za usimamizi zinawezesha kuimarika miundombinu ya mawasiliano na upatikanaji wa huduma.

Mamlaka inashajihisha upatikanaji wa mawasiliano ya kasi, inawezesha ufanisi wa mifumo ya malipo kielektron-biki na uwepo wa utambulisho wa watumiaji huduma.

TCRA iliunda minada ya masafa kwenye bendi muhimu mwaka 2018 na 2022 ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za intaneti ya kasi.

Huduma za pesa kwa simu za mkononi zimefungua fursa kwa watu wengi. Usajili wa laini za simu kibiometria unawapatia Watanzania vitambulisho vya kipekee kidijitali na pia umeongeza Imani ya watumiaji kwenye miamala na huduma za kielektroniki.

TCRA ilianzisha shughuli ya kurekebisha kanuni za leseni za huduma za mawasiliano ya kelektroniki na posta mwaka 2022. Hatua hii, imeongeza fursa kwa wajasiriamali kwenye sekta ndogo za Posta na Utangazaji na kwenye utoaji huduma kupitia mitandao ya mawasiliano ya simu. Kanuni zimeanzisha aina mpya ya leseni zinazowezesha kutoa huduma za biashara mtandao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Kuwe Bakari anaeleza kwamba jamii iliyojipanga vizuri na inayojishughulisha inaweza kujenga Uchumi shirikishi kupitia mifumo ya mawasiliano ya simu na intaneti ya ubora wa juu, inayoaminika, nafuu na inayopatikana sehemu nyingi.

TCRA pia imeanzisha utaratibu wa kutoa rasilimali za mawasiliano kama vile masafa na namba kwa wabunifu ili kujaribu uvumbuzi wao. Lengo ni kujenga ujasiliamali na kupanua wigo wa huduma za mawasiliano.

Hivi karibuni, imeanzisha mpango wa kuendeleza vilabu vya kidijitali kwenye shule na vyuo ili kujenga mwelekeo tawala wa masuala ya kidijitali kwa vijana.

# Tunu za Usimamizi na Ustawi wa Watanzania

Na Mwandishi wetu

**Sehemu hii inaangalia mipango ya kuimarisha Usalama wa Watumiaji na Mipango ya Mamlaka hiyo kusimamia teknolojia zinazoibuka**



*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akikabidhiwa kutoka kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye Kishikwambi yenye taarifa kuhusu minara ya simu milioni moja inayojengwa maeneo ya vijijini nchini Tanzania kupitia ruzuku za Serikali zote kufanya kazi kwa pamoja ili kuharakisha maendeleo ya uchumi wa kidigitali.*

TCRA ilikabili changamoto mojawapo ya mawasiliano mwaka 2009 kwa kuanzisha usajili wa laini za simu. Lengo lilikuwa ni kuongeza uimara wa matumizi, kuendeleza mtumizi sahihi na kulinda watumiaji dhidi ya wahalifu wanaotumia mitandao ya simu.

Usajili huo ulianza kupitia amri ya kiusimamizi ya TCRA kabla ya kuwekwa kisheria mwaka 2010 ilipopitishwa Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA).

Sheria iliweka masharti ya kisheria ya usajili wa laini na iliainisha adhabu kwa makosa kuhusiana na laini za simu. Pamoja na faida nyingine, usajili unahakikisha usalama na uimara wa watumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi, unafanikisha udhibiti wa uhalifu mitandaoni, na unawezesha kuwepo kanzidata ya kuaminika ya wateja waliojiunga na mitandao ya simu.

Usajili unafanyika kwa njia ya kibiometria kwa kuchukua alama za vidole za anayesajiliwa na kulinganisha taarifa zake na zilizoko NIDA.

Usajili unamwezesha kila Mtanzania aliyesajili laini kuwa na kitambulisho cha kipekee cha kidijitali,

ambacho ni muhimu katika kufanya miamala mtandaoni, kama vile kununua au kuuza bidhaa na huduma na kufanya shughuli za kibenki.

Usimamizi wa TCRA umeiwezesha Tanzania kuwa mbele ya nchi nyingi za Afrika na ukanda huu wa Afrika kwenye masuala mengi. Kwa mfano Tanzania ni nchi ya kwanza kuwa na mfumo wa malipo unaoingiliana minongoni mwa mitandao ya simu, kuanzisha na kutumia kikamilifu mfumo wa anwani za makazi na postikodi.

Aidha, nchi nyingi za Afrika zinakuja TCRA kujifunza kuhusu wa mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu (TTMS) na mfumo wa usalama mtandaoni kupitia chombo cha kitaifa kinachoshughulikia masuala ya usalama wa mitandao, na matukio ya usalama mtandaoni Tanzania (TZ-CERT) ambacho kiko TCRA.

Tarehe 31 Desemba 2014, Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza Afrika Kusini mwa Sahara upande wa bara kuzima mitambo ya utangazaji wa televisheni ya analojia kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ITU) ya 17 Juni 2015.

Kwa mujibu wa Fahirisi ya Kimataifa ya Usalama Mtandaoni iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ITU), Tanzania ilikuwa ya pili Afrika kwa Usalama Mitandaoni hadi mwaka 2020. Kung'ara huku kumetokana na hatua za kisheria na kiusimamizi zinazoleta ufanisi.

Mawasiliano kupitia simu za mkononi yamewezesha kwa kiasi kikubwa kuendelezwa kwa mkakati wa serikali mtandao nchini. Tanzania ilianzisha Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) mwaka 2012 kusimamia shughuli za kiserikali zinazofanywa kielektroniki na kuratibu mipango na viwango vya uendeshaji wa serikali-mtandao..

Ingawaje ukuaji huu wa kasi wa huduma zinazowezeshwa na TEHAMA umeathiri shughuli za kawaida za posta, ikiwemo kushuka kwa idadi ya barua na vitu vinavyosafirishwa kwa posta ya taifa, serikali imeweka mikakati ya kuinusuru taasisi hiyo.


Pamoja na TCRA kupanua wigo wa leseni kuwa na zile za biashara mtandao, ambazo zinahusisha kufikisha vifurushi kwenye makazi na ofisini, Posta ya Umma imepewa majukumu ya kuwa kituo cha huduma.

Hivi karibuni Serikali, kupitia mpango wa Tanzania wa Kidijitali, imeanzisha utaratibu wa kutoa huduma zake na za umma kupitia kituo kimoja chini ya mfumo wa posta; ambao utawezesha hadi huduma 32 kutolewa ndani ya kituo kimoja.

Mwaka 2012 TCRA ilibuni na kuongoza mipango ya kuanzisha mpango wa postikodi na anwani za makazi. Mfumo huu unahusisha matumizi ya majina ya mitaa au meneo na kutambua majina ya maeneo husika ili kufanikisha usambazaji wa barua, vifurushi na vipeto. Mfumo huu unafanikisha shughuli za taasisi za dola zinazotaka kuwasiliana na wananchi kwa sababu mbalimbali kama vile kodi, huduma za afya, huduma za zimamoto na dharura nyingine. Mfumo unainua ubora wa huduma za kusambaza barua, vifurushi na vipeto nchini na kimataifa kati ya Tanzania na nchi nyingine.

Aidha umewezesha kuanzishwa kanzidata ambayo inaweza kutumiwa na wafanyabiashara kama nyenzo muhimu ya kutangaza biashara zao na kwa tafiti za takwimu. Vile vile unatarajiwa kuboresha makazi ya watu Tanzania, na ni nyenzo inayoendana na mkakati wa serikali wa kutokomeza umaskini na kuboresha mipango vijijini.

Postikodi na anwani za makazi vimeenea Tanzania nzima. Mfumo huu ulichangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha msuala ya usambazaji wa vifaa na kusafirisha wahusika hadi kwenye maeneo mengi.



Utafiti uliofanywa na TCRA mwaka 2019 kuhusu matumizi ya mfumo huu katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Zanzibar na maeneo ya Pemba ulionyesha kwamba asilimia 66 ya watu, ikiwa ni pamoja na asilimia 93 ya madereva wa teksi, bodaboda na bajaji walikuwa wanatumia mfumo huu kwenye shughuli zao za kila siku.

# Vifaa vya mawasiliano vilivyounganishwa hadi Desemba 2023

**85.62%**
Ueneaji wa simu za kiganjani

**32.13%**
Ueneaji wa simu janja

| Aina ya kifaa | Idadi ya vifaa | **Ueneaji** (asilimia) |
|---|---|---|
| Simu za mkononi/simu za kawaida | 52,862,548 | 85.62% |
| Simu janja | 19,835,530 | 32.13% |
| Vifaa vya mkononi | 1,698,654 | 2.75% |
| Modemu | 584,323 | 0.95% |
| 'Portable' (pamoja na PDA) | 72,576 | 0.12% |
| Vishkwambi | 401,343 | 0.65% |
| Moduli | 58,209 | 0.09% |
| 'WLAN Router' | 101,027 | 0.18% |
| 'Dongle' | 101,027 | 0.16% |
| Vifaa vinavyowasiliana vyenyewe (IoT Device) | 95,336 | 0.15% |
| Vifaa kwenye magari | 18,835 | 0.03% |
| Vifaa vinavyovaliwa (wearable) | 6,724 | 0.01% |
| Vifaa vya kuchakata data moja kwa moja(Device for the Automatic Processing of Data (APD) | 1441 | 0.0023% |

TCRA imesawanisha mipango yake na ile ya kitaifa, ikiwemo ile ya serikali, ambayo inatekeleza Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025 ina malengo ya kuibadili Tanzania kidijitali na imeainisha maeneo 12 ya kimkakati kuimarisha mawasiliano na kuelekea uchumi wa kidijitali ifikapo 2025.

Malengo hayo ni kuongeza mchango wa sekta ya mawasiliano kwenye pato la Taifa kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA; kubuni na kutekeleza mikakati ya kuweka mazingira bora ya ushindani na udhibiti katika sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi zaidi wamudu gharama za mawasiliano na kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya kasi kufikia asilimia 80 ya Watanzania mwaka 2025.

Mengine ni kuongeza watumiaji wa intaneti hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2025; kuanzisha huduma za mawasiliano za intaneti ya kasi katika maeneo ya umma yakiwemo maeneo ya hospitali, taasisi za elimu na vituo vya usafiri hadi kufikia asilimia 40 mwaka 2025 na kuendeleza mtandao inayozingatia usalama wa mifumo na taarifa za serikali pia ni baadhi ya mikakati.

Mipango mingine ni kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za serikali kwa umma kwa kuanzisha vituo vya huduma ili kuongeza ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za serikali.

Lengo ni kuwarahisishia watumishi wa umma utendaji kazi na kuwapatia wananchi huduma kwa urahisi na ufanisi.

Vilevile kuna azma ya kuunganisha taasisi za Serikali na miundombinu ya mtandao wa kasi mkononi ili kupatikana maeneo yote na kuweka mazingira wezeshi ya kuanzisha viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya TEHAMA vyenye uwezo wa kutoa ajira kwa wananchi walio wengi na kuzalisha vifaa vitakavyotumika ndani na nje ya nchi.

Ujenzi wa viwanda vya kuchakata taka za kielekroniki ili kudhibiti uharibifu wa mazingira pia uko kwenye ilani ya CCM.

TCRA imejizatiti kufanikisha mipango hiyo.

Ni dhahiri kuwa mipango ya hivi karibuni ya kuongeza wigo wa masafa kwa watoa huduma na kujenga minara ya mawasiliano ya simu vitaharakisha kufikiwa lengo hilo. Serikali, kupitia TCRA ilinadi masafa katika bendi nne zinazovutia zaidi  watoa huduma Tanzania kwa dola za Kimarekani milioni 187.

Mnada huo, uliofanyika kupitia mchakato uliosimamiwa na  wataalamu wa ndani wa msimamizi wa sekta ya mawasiliano umeweka viwango vya rejea ya busara, unyoofu, ushirikiano na wadau na utekelezaji wa sera za kisekta. masafa yaliyouzwa ni kwenye  vitalu 11 vya masafa kwenye bendi ya megahezi (Mhz) 700z Mhz 2300, Mhz 2600 na Mhz 3500.

Masafa kwenye bendi ya Mhz 3500 yanapendelewa zaidi katika utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu na vifaa vya mkononi kwa kutumia teknolojia ya 5G, yaani uzao wa tano wa teknolojia za mawasiliano, ambao unatarajiwa kuwa mhimili mkubwa kwenye mkakati wa Tanzania wa kuweka misingi imara ya kujenga uchumi wa kidijitali ifikapo mwaka 2025.

Serikali, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSF) inatekeleza mradi wa kujenga na kuboresha zaidi ya minara 1,000 ya mawasiliano ya simu za mkononi nchini kote. Mradi huu, utawezesha Watanzania milioni tatu kupata huduma za intaneti kwa mara ya kwanza.



Kipindi hiki na kijacho kitashuhudia mabadiliko na maendeleo ya kasi katika TEHAMA.

Teknolojia zinazoibuka ni pamoja na Mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi ambazo kwa kawaida zinahitaji akili na utashi wa binadamu; matumizi ya maroboti na matumizi ya mifumo ya kompyuta kuonyesha hali halisi ya maisha.

Nyingine ni matumizi ya seti kubwa za data zinazoweza kuchambuliwa ili kuonyesha mwelekeo, hasa kuhusiana na vitendo vya binadamu (big data); mambo yanayowezesha matumizi ya data kuboresha uwezo wa kompyuta kufanya mambo mbalimbali (machine learning); na vitu kuwasiliano vyenyewe kupitia mfumo wa intaneti.

TCRA imeandaa miongozo ya kusimamia teknolojia mpya. Kwa mfano, mpango wa namba wa kitaifa una namba kwa ajili ya mwasiliano ya mashine kwa mashine.

Pamoja na hili, TCRA inatekeleza, kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) zimeungana ili kutoa rasilimali za mawasiliano bila malipo kwa kampuni zinazochipukia katika sekta ya teknolojia za kidijiti. Hatua hii inalenga kuweka mazingira bora ya kuvutia uvumbuzi wa kidijiti nchini na kuhakikisha kuwa kampuni hizo zina nafasi ya kukua na kufanikiwa.

Mpango huo, unaolenga kuwapa wabunifu zana wanazohitaji kwa majaribio ya huduma zao kwa kipindi maalum, unatarajiwa kuendeleza na kubadili mazingira ya TEHAMA Tanzania. UK 19

# Mfumo wa leseni ulivyochochea huduma za mawasiliano

Na Mwandishi wetu

**Makala hii inapitia mfumo wa leseni ulianzishwa 2005 na namna ulivyosukuma mandeleo ya sekta**

Kama sehemu ya maono yake, mwaka 2005 TCRA ilianzisha mfumo wa leseni wenye muingiliano wa teknolojia. Mfumo huo, unaojulikana kwa kifupi kama CLF, kifupisho cha converged licencing framework, umechangia kwa kiasi kikubwa kuendelea, kuenea na kuongezeka kwa watoa huduma za mawasiliano, aina ya huduma na idadi ya watumiaji. Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kanda ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini kuweka na kutekeleza mfumo huu.

CLF ilianzishwa kwa kuzingatia muingiliano wa teknolojia. Mfumo unamruhusu mwenye leseni ya huduma husika ya mawasiliano kuchagua aina ya teknolojia au huduma zinazojitokeza kwenye sekta bila kulazimika kuomba upya leseni kwa eneo husika.

Mfumo wa CLF una aina nne za leseni, kila moja ikiwa na vipengele vinne vya masoko, yaani kimataifa, taifa, mkoa na wilaya. Leseni hizo ni Huduma ya Mifumo Tumizi, Huduma ya Mtandao, Miundombinu ya Mtandao na Huduma ya Maudhui.

TCRA inatoa leseni za watoa huduma za utangazaji wa televisheni kutumia mifumo ya ardhini, wanaotumia mifumo ya setilaiti na wanaotumia waya kufikisha huduma kwa wateja. Leseni za maudhui kwa waya ziko hadi ngazi ya kata.

Mapema mwaka huu, Kanuni za Leseni zilirekebishwa na kuanzisha leseni za ziada chini ya makundi haya ya leseni. Mfano wa nyingezo ni ile inayowezesha utoaji huduma za maudhui ya elimu na biashara mtandao.

Huduma za maudhui zinajumuisha utangazaji wa redio na televisheni na huduma mpya kama vile kuchapisha taarifa kupitia mtandao.

Pamoja na leseni chini ya mfumo wa CLF, TCRA pia inatoa leseni ya Posta ya Taifa, kusafirisha vifurushi na vipeto, kutumia masafa, kutumia namba za mawasiliano ya simu na intaneti pamoja na za tovuti kwa kutumia kikoa cha taifa cha .tz.

Pia kuna leseni kwa wanaoingiza vifaa vya mawasiliano kutoka nje ya nchi, wanaouza, wanaosambaza na wanaofunga na kutengeneza vifaa vya mawasiliano. Vile vile kuna idhini ya kuthibitisha ubora wa vifaa vya mawasiliano vinavyoingizwa na kutumiwa Tanzania.

**Jedwali 1: Mwenendo wa hivi karibuni wa usajili laini za simu za mkononi na akaunti za pesa kwa simu.**

| Mwaka | Akaunti | Ongezeko | Asilimia ya ongezeko (%) | Laini za simu zilizosajiliwa | Ongezeko | Asilimia ya ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Desemba 2019 | 25,864,318 | - | - | 47,685,232 | - | - |
| Desemba 2020 | 32,268,630 | 6,406,502 | 24.76 | 51,220,233 | 3,535,001 | 7.41 |
| Desemba 2021 | 35,285,767 | 3,017,137 | 9.35 | 54,044,384 | 2,824,151 | 5.51 |
| Desemba 2022 | 40,953,496 | 5,667,729 | 16.06 | 60,192,331 | 6,147,947 | 11.37 |
| December 2023 | 52,875,129 | 11,921,633 | 29.10 | 70,300,000 | 10,107,669 | 16.79 |

Tangu kuanzishwa mwaka 2003 hadi Desemba 2023 TCRA imetoa leseni mbalimbali kama:-

- Miundombinu ya Mawasiliano **36**
- Utumiaji wa Miundombinu ya Mtandao **17**
- Huduma Tumizi za Mawasiliano **142**
- Televisheni za mfumo wa ardhini **69**
- Televisheni za mtandaoni **222**
- Televisheni njia ya waya **56**
- Redio za mfumo wa kawaida **234** na redio za mtandaoni **6**

Kundi la leseni za maudhui mtandaoni lilianzishwa 2018.

Leseni za Ufungaji na Utengenezaji, Uingizaji na Usambazaji wa Vifaa vya Simu; madishi ya VSAT; na Masafa ya VHF/HF ziko 1,642.

Mwaka 2007 Tanzania ilianzisha huduma za kifedha kidijitali. Ilikuwa miongoni mwa nchi chache za Afrika ambazo mifumo ya kifedha kwa kutumia vifaa vya Mawasiliano kiganjani inatumika kwa kiwango kikubwa, kiasi cha kusaidia kutatua changamoto za utoaji na upatikanaji wa huduma.

Kupitia huduma hii, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejizolea sifa kubwa, hadi kwenye Taasisi ya Mawasiliano ya Umoja wa Mataifa (ITU) nchini Uswizi kwa Kuingiza Wananchi wake kwenye Mfumo jumuhishi wa Kiuchumi na kifedha.

Usimamizi wa masuala ya fedha mtandao unafanywa na Benki Kuu Tanzania (BOT). TCRA inapanga Mifumo na kutoa namba zinazotumika katika mawasiliano pamoja na namba fupi (misimbo) zinazotumika katika kufanya miamala ya kifedha na kuwezesha huduma nyingine za ziada.

Akaunti za pesa kupitia simu zimeongezeka kwa kasi. Taarifa ya mwaka 2019/2020 ya Benki Kuu ya Tanzania inaonyesha kwamba miamala ya kifedha kupitia simu za mkononi imekua kwa asilimia 21.8 kwa ukubwa na asilimia 8.9 kwa thamani ya miamala ukilinganisha na 2018/2019.

Huduma za fedha mtandao zimezalisha ajira nyingi, zikiwemo za wakala. Vilevile benki nyingi zimeboresha na kurahisisha huduma zake ambapo zinawatumia watoa huduma hawa kama wakala wao ili kufikisha huduma za kibenki karibu na wateja wao.


Pamoja na kuleta ufanisi, huduma za fedha kupitia simu za mkononi pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi, hasa baada ya serikali kuanzisha mfumo wa malipo ya kiserikali mtandaoni (GePG).

Mwaka 2016 Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza barani Afrika na Ulimwenguni kuwa na mfumo kamili uliowezesha muingiliano wa mitandao ya fedha kupitia simu za mkononi.

Matokeo ya yote yaliyofanyika ni kuwa Uwiano wa viashirio vingi vya maendeleo ya mawasiliano viko juu ya asilimia 50, isipokuwa kwa upande wa kuenea kwa simu zenye uwezo mkubwa, au simu janja; ambazo ni muhimu katika kuendeleza matumizi ya intaneti kupitia simu za mkononi.

Uchambuzi wa viashirio na uwiano wake kwa idadi ya watu Tanzania unaonesha kuwa mawasiliano ya simu za 2G, yaani uzao wa kidijitali na unaohakikisha ubora zaidi wa sauti na ujumbe mfupi, yaani meseji umefikia asilimia 98. Mawasiliano ya simu uzao wa 3G uko asilimia 86. Uzao wa 3G unawezesha watumiaji kupata huduma zinazowezeshwa na 2G, na pia kutuma na kupokea barua pepe kwa wingi mara moja.

Uzao wa 4G umeenea asilimia 79. Huu unawezesha maongezi, meseji, data, video, picha na hata televisheni kupitia simu ya mkononi. Simu janja zimeenea kwa asilimia 32 tu ya watu.




Takwimu za Desemba 2023 zinaonesha kulikuwa na laini milioni 70.3 zilisajiliwa hadi kipindi hicho, kulinganisha na laini milioni 1.2 zilizokuwepo 2003.

Matumizi ya simu yanasukuma maendeleo ya jamii na kuongeza kasi ya maendeleo ya Taifa. Utafiti uliofanywa kwenye matumizi ya simu za mkononi katika nchi 92 ikiwemo Tanzania mwaka 2019 umeonyesha kwamba ongezeko la simu za mkononi moja kwa watu 100 linaongeza ukuaji wa pato la taifa kwa asilimia 0.6 kila mwaka.

Simu za mkononi zimewezesha kujengeka kwa jamii inayoshiriki katika mfumo wa kifedha, zimewezesha matumizi ya huduma za kielektroniki. Mifumo ya kidijitali imewezesha kuenea kwa huduma za jamii, kiuchumi na utawala kupitia mitandao.

Kipindi cha janga la UVIKO-19 kilionesha dhahiri namna mawasiliano yalivyorahisisha shughuli za kiofisi, kwa kuwezesha watu kufanya kazi na kushiriki mikutano na vikao wakiwa nyumbani au nje ya sehemu za kazi.

Kuongezeka kwa laini za simu za mkononi kumepanua upatikanaji wa huduma hizo kwa wingi zaidi miongoni mwa wananchi ndani ya miaka  mitano iliyopita.

## Jedwali 3: Vidokezi vingine vinavyoakisi ukuaji wa sekta (Septemba-Desemba2023)

| Maelezo | Idadi | Maelezo |
|---|---|---|
| Leseni zilizotolewa kipindi hiki | 180 | Zinafikisha jumla ya leseni 2,546 zilizotolewa na TCRA tangu 2003. |
| Vikoa vya Tanzania (Dot.tz) vilivyosajiliwa | 445 | Jumla ya vikoa vilivyosajiliwa hadi Desemba ni 29,006 |
| Ithibati zilizotolewa kwa wasajili vikoa | Nne (4) | Wasajili 77 wamepata ithibati hadi sasa |
| Vyeti vilivyotolewa kwa vifaa vya mawasiliano vilivyoidhinishwa kutumika Tanzania | 39 | Kulikuwa na zaidi ya vifaa 1,000 kutoka kwa watengenezaji nchi mbalimbali |
| Laini za simu za mkononi zilizosajiliwa | Milioni 70.3 | Ongezeko la asilimia  4.7 kulinganisha na Septemba ambako zilikuwa milioni 67.1 |


Kuna mipango mingi ya kutumia TEHAMA kwenye huduma mbalimbali za kijamii. Kwa mfano, mwaka 2020 Tanzania ilizindua kituo cha huduma za tiba mtandao(tele-medicine) katika hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, ambacho kinawezesha mabingwa wa tiba Tanzania kutoa huduma wakiwa mbali kwa wagonjwa wilayani na hata katika nchi za jirani.

Madaktari bingwa wataweza kuhudumia wagonjwa na kutoa ushauri kwa watendaji wa afya wilayani na mikoani wakiwa mbali.

Aidha, ukuaji wa matumizi ya data unafanikisha mawasiliano ya kibinafsi na kibiashara.

Intaneti imewezesha watanzania kujenga uhusiano kupitia mitandao ya kijamii, kupata elimu na ujuzi, kujiongezea kipato kwa kutanua wigo wa wateja kupitia biashara mtandao, kupunguza kero ya upatikanaji huduma kama vile malipo ya serikali na kodi mbalimbali na kadhalika.

Vilevile intaneti inaendeleza ufanisi wa taasisi na kuwezesha kasi ya kubadilishana taarifa.



# Takwimu sekta ya Mawasiliano

## Watumiaji wa huduma za simu


| Septemba 2023 | Desemba 2023 | |
|---|---|---|
| Milioni **67.1** | Milioni **70.3** | **4.7%** |

### Idadi ya watumiaji wa simu mwezi Oktoba - Desemba 2023

| | OKTOBA | NOVEMBA | DESEMBA |
|---|---|---|---|
| **AIRTEL** | 18,636,019 | 18,932,628 | 19,146,016 |
| **HALOTEL** | 8,123,970 | 8,192,481 | 8,529,919 |
| **TIGO** | 18,526,497 | 18,923,699 | 19,698,263 |
| **TTCL** | 1,621,247 | 1,634,231 | 1,644,194 |
| **VODACOM** | 20,917,366 | 21,127,719 | 21,272,484 |
| **TOTAL** | **67,825,099** | **68,810,758** | **70,290,876** |

**1.8%** **Wastani wa ongezeko la watumiaji kila mwezi kati ya Oktoba na Desemba 2023**

## Mgawanyo wa soko la watumiaji wa mitandao ya simu mwaka 2023





### Mwenendo wa watumiaji wa mitandao ya simu kwa miaka mitano

| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Watumiaji wa simu za mkononi** | 47,685,232 | 51,220,233 | 54,044,384 | 60,192,331 | 70,215,144 |
| **Watumiaji wa simu za mezani** | 76,288 | 72,469 | 71,834 | 84,696 | 75,132 |
| **Jumla ya watumiaji** | 47,763,539 | 51,294,722 | 54,118,239 | 60,279,049 | 70,292,899 |
| **Kuenea kwa huduma** | **78%** | **81%** | **88%** | **98%** | **111%** |

# Watumiaji wa huduma za kifedha kwa njia ya simu

Matumizi ya huduma za kifedha yanahusu idadi ya kadi za simu zilizo hai na akaunti za huduma ya pesa za simu ambazo zimerekodi shughuli/zimetumika angalau mara moja katika miezi mitatu iliyopita





2.9%

## Watumiaji wa huduma za kifedha kwa njia ya simu (idadi ya akaunti)

| | OKTOBA | NOVEMBA | DESEMBA |
|---|---|---|---|
| Airtel Money | 11,093,817 | 11,238,059 | 11,166,688 |
| Halopesa | 3,934,965 | 3,985,603 | 4,034,261 |
| Tigo Pesa | 15,801,524 | 16,019,568 | 16,260,532 |
| T-Pesa | 1,350,412 | 1,360,058 | 1,370,470 |
| M-Pesa | 19,180,295 | 19,466,821 | 20,043,178 |
| **JUMLA** | **51,361,013** | **52,070,109** | **52,875,129** |

## Mgawanyo wa soko la watoa huduma wa kifedha kwa njia ya simu

**90%** Soko la huduma la kifedha kwa njia ya simu ni lenye ushindani mkubwa ambapo Tigo Pesa, M-Pesa, na Airtel Money wakidhibiti asilimia 90 ya soko kwa watumiaji, huku M-Pesa ikiwa kinara kwa kuwa na asilimia 38 ya watumiaji.




## Mwenendo wa miamala ya kifedha kwa njia ya simu kwa miaka mitano

| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watumiaji | 25,864,318 | 32,268,630 | 35,285,767 | 40,953,496 | 52,875,129 |
| Idadi ya miamala | 3,021,142,958 | 3,412,210,062 | 3,752,084,894 | 4,195,899,414 | 5,273,086,154 |
| Wastani wa idadi ya watumiaji na miamala | 117 | 106 | 106 | 102 | 100 |

# Matumizi ya Intaneti

## Je, wajua?

Matumizi ya huduma ya Intaneti ya simu na Intaneti ya nyumbani, na njia kuu ya kupata intaneti, unafafanuliwa kama idadi ya jumla ya simu kadi ambazo zimefikia na kutumia huduma za intaneti katika miezi mitatu iliyopita, bila kujali teknolojia iliyotumika kama ni (**FTTX, GPRS, 3G, 4G, au 5G).**"

**Milioni 35.9**

Watumiaji wa huduma za intaneti hadi kufikia Desemba 2023, ikiwa ni ongezeko la **4.1%** kutoka idadi iliyorekodiwa wakati wa robo iliyomalizika Septemba 2023

## Watumiaji wa huduma za intaneti kwa mwezi

| | OKTOBA | NOVEMBA | DESEMBA |
|---|---|---|---|
| Inatenti kwenye simu | 34,751,832 | 35,626,666 | 35,815,632 |
| Intanenti isiyo ya waya | 7,995 | 7,937 | 8,315 |
| Intaneti ya waya | 52,912 | 59,067 | 61,645 |
| **JUMLA** | **34,812,739** | **35,693,670** | **35,885,592** |

## Matumizi ya intaneti kwa mwezi

Petabaiti **92**

**Septemba 2023**

Petabaiti **104**


**Desemba 2023**

**13%**

## Mwenendo wa watumiaji wa intaneti kwa miaka mitano

**9.8%**

Wastani wa ukuaji wa watumiaji wa intaneti kwa kipindi cha miaka mitano



# Kilabu za Kidijiti kuibadili Tanzania




Tanzania imelenga kujenga utamaduni wa ubunifu katika masuala ya kidijitali ili kujenga jamii inayotumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwenye shughuli mbalimbali.

Katibu Mkuu, Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Bw. Mohammed Khamis Abdulla amesema jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kwamba Wizara yake imeweka malengo ya kuchochea talanta na bunifu kutoka kuanzia shule za awali na msingi.

Akizindua kitabu chenye utaratibu wa kuanzisha na kuratibu 'Klabu za Kidijiti Tanzania', kilichoandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ameeleza kwamba Wizara hiyo, kupitia Tume ya TEHAMA, imeanza taratibu za kuanzisha vituo vya ubunifu nchini kwa vijana wote bila kujali elimu waliyonayo.

"Uwepo wa klabu za Kidijiti zitawasaidia vijana kuimarisha ubunifu, uvumbuzi na kufanya ndoto zao kuwa za kweli na hatimae kukuza tamaduni ya ubunifu nchini" alifafanua.

Ametaja faida za klabu hizo kuwa ni kupunguza pengo la ujuzi wa kidijiti,kuongeza stadi za Kidijiti miongoni mwa vijana, kuongeza na kukuza ajira na kuhamasisha ubunifu kwa wanafunzi. Vilevile zinawajengea vijana fikra zenye mantiki, na kutatua changamoto zinazowakabili.

Klabu za Kidijiti, ambazo ni sehemu ya mkakati wa kujenga Tanzania ya Kidijitali, ni majukwaa ya hiari yanayowakutanisha wanafunzi wa rika moja kupata uelewa na kuhamasishana juu ya TEHAMA, uchumi wa kidijiti na fursa zake.

Mfano, wanafunzi wanakutana na kujadili kuhusu changamoto mbalimbali zilizopo kwenye maeneo yao na jinsi ya kuzitatua kwa kutumia TEHAMA, matumizi sahihi ya mtandao, ubunifu na jinsi ya kuandaa programu tumizi Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari amesema mpango huo unatokana na azma ya Mamlaka kuongeza hamasa na uelewa zaidi wa fursa zilizopo, na kuongeza uwezo na weledi wa vijana kushiriki uchumi wa kidijiti kikamilifu, kuanzia shule za awali hadi ya Vyuo Vikuu.

Klabu hizo zinatarajiwa kuwaongezea wanafunzi motisha na kuwahamasisha wanafunzi kupenda na kusoma sayansi, teknolojia, uhandisi, hisabati na masomo mengine, hivyo kukuza fikra za kitaalamu, ubunifu, na uvumbuzi, alifafanua.

> *Kwa kufanya hivyo; tunaamini, klabu hizi zitasaidia kuendeleza ujuzi na maarifa ili kukabiliana na changamoto zilizopo na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi, kisayansi, teknolojia, na jamii kwa ujumla.*
>
> Dkt. Jabiri K Bakari

TCRA itashirikiana na wadau wa elimu kwenye ngazi zote wakiwemo walimu na wanafunzi kutoka vyuo vya kati na vikuu katika kufanikisha mpango huu, amesema na kuongeza kuwa kitabu hicho kitaboreshwa kulingana na ukuaji wa teknolojia na matumizi yake.

## TCRA kituo cha uzoefu Afrika



*Ujumbe wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Simu na Posta kutoka nchini Mali (AMRTP) ukiwa TCRA hivi karibuni ambako walijifunza na kubadilishana uzoefu kwenye maeneo kadhaa, yakiwemo huduma za pesa kupitia mitandao, uthibitishaji wa vifaa vya nawasiliano na usimamizi wa rasilimali zinazotumika kweye mawasiliano ya intaneti.*

*Ujumbe huo (pichani kushoto) uliongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Simu na Intaneti cha mamlaka hiyo, Bwana Cisse Ahmadou Dit Adi. Katikati ni Mkurugenzi wa TCRA wa Leseni na Ufuatiliaji, Bwana John Daffa na kulia ni maafisa wengine wenyeji.*



*Wataalamu wa Tume ya Mawasiliano Eswatini –(ESCCOM) wakipata maelezo kuhusu usimamizi wa shughuli za utangazaji walipotembea TCRA kwa mafunzo. Ujumbe uliongozwa na Meneja wa Mawasiliano wa Tume hiyo, Bwana Vusi Khumalo. Katikati ni Mkurugenzi wa TCRA masuala ya Leseni na Ufuatiliaji, Bwana John Daffa*

## Redio wilayani kuendeleza maadili ya Kitanzania

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) naratibu programu maalumu ya kuandaa vipindi vya maadili vitakavyorushwa na vituo vya Utangazaji 150 vyenye leseni ya kiwilaya ili kujenga nchini jamii yenye maadili mema.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri K. Bakari amesema chini ya mpango huo; unaotekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum; vituo 14 vyenye leseni ya Kitaifa vinarusha vipindi vinavyotoa elimu ya malezi bora ya familia na vijana.

Lengo ni kuimarisha utoaji elimu na kujenga jamii inayozingatia maadili, mila desturi na utamaduni wa Mtanzania, ameeleza na kuongeza kuwa mpango huo pia utahusisha kuandaa na kutoa katuni za watoto na ngoma za asili.

Mpango wa uandaaji wa ngoma za asili umeshirikisha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Dkt. Jabiri ameongeza kwamba hatua hizi zimechukuliwa kama sehemu ya jitihada za kupambana na maudhui yanayotoka nje ya nchi ikiwa ni pamoja na katuni za watoto zisizo na maadili ya Kitanzania.

Ametoa rai kwa vyombo vya utangazaji kuendelea kuzingatia sheria, kanuni na weledi katika kutoa maudhui.

Amesisitiza kuwa TCRA ina wajibu wa kuhakikisha kuwa maudhui yanayorushwa na vituo vya Utangazaji yanazingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari na pia havikiuki Sheria na Kanuni za Utangazaji.

TCRA inahimiza utengenezaji, uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya ndani, ameongeza.

Wakati huohuo TCRA imekutana na watengenezaji maudhui wanaojitegemea na kuwataka kushirikiana ili kuboresha shughuli zao.



*Wawakilishi wa Chama cha Wazalishaji Huru wa Maudhui Tanzania (TAIPA) wakiwa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri K.Bakari (wa pili kushoto waliokaa) baada ya mkutano wa mashauriano hivi karibuni.*

# Majiji ya kidijitali ajenda mkutano wa ITU Arusha

Na Mwandishi wetu

Wataalamu wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wa nchi mbalimbali, chini ya utaribu wa Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) wameku tana jijini Arusha hii karibuni kujadili masuala saba yanayohusiana na uendelezaji majiji ya kisasa.

Mkutano huo wa wataalamu wanaounda kundi namba 20 la ITU la wataalamu wanaoshughulikia masuala ya vifaaa vinayojiendesha vyenyewe kupitia intaneti, na majiji ya kisasa, ulisisitiza umuhimu wa kuweka misingi itakayohakikisha uendelevu wa majiji ya kisasa.

Mkutano pia ulijadili matumizi ya TEHAMA katika shughuli za uendeshaji na uzalishaji. Masuala yaliyojadiliwa ni usimamizi wa taarifa, mifumo ya usafiri inayotumia TEHAMA, kilimo ufugaji bora kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Tanzania inatekeleza mpango wa kubadili majiji ya Dodoma, Arusha na Mbeya kuwa ya kisasa, hivyo kujiunga na majiji maarufu barani Afrika kama vile Cape Town Afrika Kusini ambayo yana hadhi hiyo.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye ameliambia Bunge jijini Dodoma Mei 19 mwaka huu kwamba wizara yake itafanya tathmini ya kuyafanya majiji hayo kuwa ya kisasa kidijitali.

Madhumuni ni kutabadili maisha ya wakazi wa majiji hayo, aliongeza.

Majiji ya kisasa kidijitali yanakuwa na mifumo ya kielektroniki inayosimamia huduma za umma na za kiusalama ikiwani pamoja na kuwezesha taa za kuongoza magari kubaini mwelekeo wa foleni, mfumo wa kielektroniki wa kukusanya data za matumizi ya umeme, maji na hudma za taka.

Ili jiji liwe la kisasa kidijitali, linahitaji wakazi wake kuwa na uelewa kwenye matumizi ya huduma za kidijitali. Pia linahitaji miundombinu imara, upatikanaji wa masafa ya mawasiliano ya kasi yanayowezesha intaneti ya uhakika, vyanzo vya nishati vinavyoaminika na miundombinu na mifumo wa usafiri.

